*Kioo cha Lugha, Juz. 23(1), 86-106*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam* DOI: https://dx.doi.org/10.4314/kcl.v23i1.6

# Mbinu za Ujenzi wa Masuala ya Kiuhalisia Hakiki na Dhima zake katika Riwaya za *Kichwamaji* (1974) na *Dunia Uwanja wa Fujo* (1975)

*Tusingwire Timon*[1] *na Leonard F. Ilomo*[2]

## Ikisiri

Mtindo wa uhalisia hakiki unahusu uandishi wa kazi za fasihi ambapo masuala anuwai ya kijamii hubainishwa na mwandishi pasipo hofu yoyote. Mwandishi anapotumia mtindo huu katika uandishi wake huchambua maovu yaliyopo kwenye jamii na kuyaweka wazi bila kificho chochote. Wakati mwingine, uandishi wa namna hii huhatarisha usalama wake. Hivyo, ni waandishi wachache sana wenye uthubutu huo hasa kama maovu hayo yanawahusu wenye mamlaka moja kwa moja. Makala hii imechunguza mbinu zinazotumika kujenga masuala ya kiuhalisia hakiki katika uandishi pamoja na dhima za mtindo huo katika riwaya za *Kichwamaji* (1974) na *Dunia Uwanja wa Fujo* (1975) zilizoandikwa na Euphrase Kezilahabi. Data za utafiti zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya usomaji makini wa matini teule. Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Uhalisia kwa kujikita katika mkabala wake wa uhalisia hakiki. Matokeo yameonesha kwamba kuna mbinu tano zinazotumika kujenga masuala ya kiuhalisia hakiki kiuandishi ambayo ni majadiliano baina ya wahusika, matendo ya wahusika, uzungumzinafsiya, sitiari na uwasilishaji dhahiri. Kwa upande mwingine, dhima za mtindo huo ni kumpambanua msanii, kumtafakarisha msomaji, kujenga jamii mpya na kuibua mambo mapya katika jamii.

## 1.0 Utangulizi

Uhalisia hakiki ni mtindo wa uandishi ambao mwandishi hushambulia maovu ya jamii bila kuogopa (Gorky, 1949). Mwandishi huyu anaendelea kueleza kuwa katika mtindo wa uhalisia hakiki, mwandishi husawiri jamii iliyo nzuri, na baadaye katika jamii hiyohiyo hutokea watu ambao huharibu utaratibu ama kwa kukiuka maadili ya kidini au kutatiza hali nzuri iliyotarajiwa katika jamii husika. Kwa upande wake Mulokozi (2017), anaeleza kwamba uhalisia hakiki ni mkabala na

[1] Mhadhiri Msaidizi, Taasisi ya Taaluma za Lugha, Chuo Kikuu cha Kabale, Uganda. Baruapepe: ttusingwire@kab.ac.ug

[2] Mhadhiri, Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania. Baruapepe: leonardilomo@gmail.com

mtindo wa utunzi uliotumiwa na wahalisia wakuu wa karne ya 19-20 huko Ulaya na kwingineko duniani kuisawiri jamii. Anaendelea kueleza kuwa watunzi kama Leo Tolstoy (Urusi) na Charles Dickens (Uingereza) walikuwa wahalisia hakiki. Watunzi hao hawakuishia kuonesha tu hali kama ilivyo bali walisaili, walichambua na kukosoa hali hiyo wakiwa na lengo la kujenga jamii mpya ambayo haitakuwa na mambo yaliyosailiwa. Mulokozi anaenda mbali zaidi kwa kueleza kwamba katika Kiswahili, watunzi kama Euphrase Kezilahabi (riwaya za mwanzo) na wengine wengi wa miaka ya 1970-1990 wanaingia katika tapo la wahalisia hakiki. Kulingana na maelezo ya Mulokozi, mtindo wa uhalisia hakiki umetumiwa pia na waandishi wa fasihi ya Kiswahili. Hata hivyo, Mulokozi haelezi namna mtindo huu unavyojengwa na dhima zake katika fasihi ya Kiswahili zaidi ya kudokeza tu ilhali mtindo huu unaelezwa na watalaamu kuwa una mchango mkubwa katika maisha ya wanajamii na katika ujenzi wa jamii kwa ujumla. Mathalani, Vasquez (1973) na Laird (2006) wakielezea mchango wa mtindo huu wa uhalisia hakiki, wanasema kuwa masuala ya kiuhalisia hakiki katika kazi za fasihi huleta athari chanya kwenye jamii na huchangia katika kuhimiza au kupuuza fikra zao, maazimio yao na maadili ya wanajamii husika. Naye Bhasker (2007) anaeleza kwamba waandishi wa kazi za kifasihi wanapoisawiri jamii kupitia mtindo wa uhalisia hakiki huwavutia watu wengi na husaidia kuibua mambo ambayo yasingeweza kusemwa au kuelezwa kupitia mtindo mwingine. Hali hii imesababisha kutofahamika kwa masuala mbalimbali yanayohusiana na mtindo huu, yakiwamo mbinu zinazotumika kuujenga na dhima zake, licha ya kuelezwa na wataalamu kwamba mtindo huu unachangia katika maisha ya wanajamii. Hivyo, kutokana na hali hii, watafiti walihamasika kuchunguza mbinu zinazotumika kujenga mtindo huu na dhima zake katika uandishi wa riwaya ya Kiswahili.

Riwaya teule za Euphrase Kezilahabi (*Kichwamaji* ya 1974 na *Dunia Uwanja wa Fujo* ya 1975) zimetumika ili kufanikisha uchunguzi wa mbinu za ujenzi wa masuala ya kiuhalisia hakiki na dhima zake katika riwaya ya Kiswahili. Mwandishi huyu aliteuliwa kwa sababu anatajwa na wataalamu mbalimbali kwamba ametumia mtindo wa uhalisia hakiki (taz. Mlacha na Madumulla, 1991; Madumulla, 2009; Mulokozi, 2017). Hivyo basi, makala hii imeonesha mbinu za ujenzi wa masuala ya kiuhalisia hakiki na dhima zake katika riwaya za *Kichwamaji* (1974) na *Dunia Uwanja wa Fujo* (1975) za Kezilahabi.

## 2.0 Kiunzi cha Nadharia Iliyoongoza Makala

Uchambuzi wa data za makala hii umeongozwa na Nadharia ya Uhalisia kwa kujikita katika Mkabala wa Uhalisia Hakiki. Nadharia ya Uhalisia ilichipuka katika karne ya kumi na tisa (19). Nadharia hii inahusishwa na waasisi mbalimbali. Wamitila (2008) anaeleza kwamba miongoni mwa waasisi wa nadharia hii ni Gustave Flaubert (1850) na Erving Goffman (1952). Wamitila anaendelea kueleza kwamba wataalamu hawa wanashikilia kuwa mtu hufikiria kwa kichwa chake,

hafikirii kwa moyo wake. Vilevile, wataalamu hawa wanaeleza kuwa Nadharia ya Uhalisia inatumika kwa lengo la kuusawiri uhalisia katika ukamilifu na wakati wake maalumu. Wanaendelea kueleza kuwa kazi ya fasihi inapaswa iwakilishe ukweli kwa kutumia maneno halisi, iwe ya kuaminika na iakisi au ioneshe hali halisi katika maisha ya mwanadamu.

Nadharia ya Uhalisia ina mikabala mbalimbali. Hata hivyo, kwa mujibu wa Mulokozi (2017) mikabala iliyokuwa na nguvu sana katika karne ya 20 ni Uhalisia Hakiki na Uhalisia wa Kijamaa. Hivyo, kulingana na mada ya makala hii tumeongozwa na Mkabala wa Uhalisia Hakiki. Mulokozi (2017) anaeleza kwamba, uhalisia hakiki ni mkabala na mtindo wa utunzi uliotumiwa na wahalisia wakuu wa karne ya 19-20 huko Ulaya na kwingineko kuisawiri jamii. Watunzi kama Charles Dickens kutoka Uingereza na Leo Tolstoy kutoka Urusi walikuwa wahalisia hakiki kwa sababu hawakuonesha tu hali halisi kama ilivyo bali walisaili, walichambua na kukosoa hali hiyo.

Aidha, Arabi na wenzake (2022) wanaeleza kwamba, uhalisia hakiki ulikuwa aina mpya ya uhalisia ambapo mwandishi hakuishia tu kuyasawiri maisha kama yalivyo bali alisawiri matatizo mbalimbali ya kijamii kwa kuyakosoa na kuyachambua. Kwa ujumla, kulingana na maelezo yaliyotolewa hapo juu, barani Ulaya uhalisia hakiki ulianza karne ya 18 na kuendelea. Kwa upande wa fasihi ya Kiswahili, Madumulla (2009) anaeleza kwamba uhalisia hakiki ulianza kujitokeza miaka ya 1970 na mwanzoni mwa miaka ya 1980 ambapo ndoto na matarajio kuhusu kuifikia nchi ya ahadi ya Azimio vilianza kufutika. Hali ya uchumi ya wananchi ilianza kudidimia waziwazi. Idadi kubwa ya vijiji vya Ujamaa na makazi mapya yaliyokuwa yameanzishwa yalianza kusuasua miaka ya 1970. Madumulla anaeleza kwamba hali hii ndiyo ilisababisha kuibuka kwa nathari bunilizi ambazo zilielekeza kidole cha mashtaka kwa viongozi wa serikali kwa uroho wao, usaliti na rushwa. Viongozi hawakutaka kuwasaidia viongozi wadogo ambao walikuwa na imani katika ujenzi wa jamii mpya ya kijamaa. Mifano mizuri ya riwaya zilizotumia mtindo huu ni riwaya ya *Nyota ya Huzuni* (1978) na *Njozi Iliyopotea* (1979). Madumulla anasema kuwa zipo riwaya zingine ambazo zilisaili hali ya maisha ilivyokuwa ikiendelea. Mifano ya riwaya hizo ni *Kichwamaji* (1974) na *Gamba la Nyoka* (1979) za Kezilahabi. Maelezo haya yanaonesha kwamba riwaya zilizotungwa miaka ya 1970 na mwanzoni mwa miaka ya 1980 hazikuishia tu kusawiri masuala ya kisiasa na kijamii bali pia zilikosoa. Msingi mkuu wa Mkabala wa Uhalisia Hakiki ni kuchambua, kusaili na kukosoa hali iliyopo katika jamii. Hivyo, ili kuchambua data za makala hii, tumejiegemeza katika msingi huo.

## 3.0 Methodolojia ya Utafiti

Kipengele hiki kimeweka bayana mbinu mbalimbali ambazo zimetumika kukamilisha ukusanyaji wa data, uchambuzi na uandishi wa makala hii. Mbinu hizo ni wango, sampuli, usampulishaji, mbinu ya ukusanyaji na uchambuzi wa

data. Mathalani, wango la utafiti lilikuwa riwaya za mwanzo (zilizoandikwa miaka ya 1970) za Kezilahabi. Uteuzi wa wango hilo uliukiliwa na mawazo ya Madumulla (2009) na Mulokozi (2010 na 2017) wanaodai kwamba, Euphrase Kezilahabi ni miongoni mwa watunzi waliotumia mtindo wa uhalisia hakiki kwenye riwaya zake za mwanzo. *Riwaya za Kichwamaji* (1974) na *Dunia Uwanja wa Fujo* (1975) ndizo zimetumika kama sampuli ya utafiti huu. Mbinu iliyotumika kupata sampuli ya riwaya hizo ni usampulishaji nasibu sahili kwa kutumia mbinu ya vikaratasi. Katika mbinu hii, vikaratasi vyenye majina ya riwaya za mwanzo za Kezilahabi viliandikwa na kukunjwa. Baada ya hapo watafiti walimuomba mwenzao achague vikaratasi viwili kati ya vinne ndivyo riwaya za *Kichwamaji* (1974) na *Dunia Uwanja wa Fujo* (1975) zilivyopatikana. Mbinu ya usomaji makini wa matini imetumika katika ukusanyaji wa data za makala hii. Kwa upande mwingine, katika uchambuzi wa data, watafiti wametumia mbinu ya uchanganuzi wa data kimaudhui. Katika mbinu hii, data zenye maudhui yanayoendana zimewekwa kwenye kundi moja.

## 4.0 Uwasilishaji wa Data na Matokeo ya Utafiti

Kulingana na mawanda ya utafiti huu na uwasilishaji wa data, matokeo ya utafiti yamegawanyika katika sehemu kuu mbili. Katika sehemu ya kwanza tumewasilisha data zinazohusu mbinu zilizotumika kujenga masuala ya kiuhalisia hakiki katika riwaya za *Kichwamaji* na *Dunia Uwanja wa Fujo*. Sehemu hiyo imewasilishwa kupitia kipengele cha 4.1. Katika sehemu ya pili tumewasilisha data zinazohusu dhima za mtindo wa uhalisia hakiki katika uandishi kupitia kipengele nambari 4.2. Udadavuzi wa sehemu moja baada ya nyingine ni kama ufuatao:

### 4.1 Mbinu ya Kiuhalisia Hakiki katika Riwaya Teule

Sehemu hii imeeleza mbinu ambazo zimetumika kujenga masuala ya kiuhalisia hakiki katika riwaya za *Kichwamaji* na *Dunia Uwanja wa Fujo*. Mbinu hizo ni majadiliano baina ya wahusika, matendo ya wahusika, uzungumzinafsiya, sitiari na uwasilishaji dhahiri. Katika uchambuzi wa mbinu hizo, tumeongozwa na Mkabala wa Uhalisia Hakiki ambao unasema kwamba, mwandishi wa kiuhalisia hakiki, haishii tu kuisawiri hali halisi ya kijamii, bali huichambua, huikosoa na huisaili hali hiyo. Ufuatao ni uchambuzi wa mbinu moja baada ya nyingine namna ilivyotumika kujenga masuala ya kiuhalisia hakiki kwenye riwaya za *Kichwamaji* na *Dunia Uwanja wa Fujo*.

#### 4.1.1 Mbinu ya Majadiliano baina ya Wahusika

Hii ni miongoni mwa mbinu ambazo zimetumiwa na mwandishi katika kujenga masuala yanayojitokeza kiuhalisia hakiki. Mwandishi amewapambanisha wahusika ili wajadiliane wao kwa wao kuhusu masuala mbalimbali. Kupitia

mazungumzo baina ya wahusika ndipo tunapata kufahamu namna mwandishi anavyochambua, anavyosaili na kukosoa masuala mbalimbali ya kijamii. Hili limesaidia kupata wazo la mwandishi kuhusiana na masuala ya kijamii ambayo ndiyo msingi wa uhalisia hakiki. Kwa mfano, katika riwaya ya *Kichwamaji* (1974), mwandishi anatuibulia masuala mbalimbali kupitia mijadala ya wahusika. Baadhi ya majadiliano baina ya wahusika yanayoibua masuala yanayojitokeza kiuhalisia hakiki katika riwaya hii ni mjadala baina ya Manase na Kazimoto ambao unatuibulia suala la kihalisia hakiki ambalo ni kifo. Kupitia mjadala huo, Kezilahabi anafanikiwa kuchambua, kusaili na kukosoa mambo mbalimbali kuhusu kifo. Mwandishi anawapambanisha wahusika hawa katika mjadala kuhusu kifo kama ifuatavyo:

> Ukweli ni kwamba sisi wanadamu tunakufa polepole. Watu wengi wanafikiri kwamba sisi wanadamu tunakufa mara moja. Hili ni jambo la uongo. Tangu mwanadamu anapozaliwa anaanza kufa polepole ingawa yeye mwenyewe anajiona yu sawa. Siku zake zinakatwa mojamoja. Kaburi ni hatua yetu ya mwisho tu. Kazimoto, tunapoishi tunakufa polepole; kwa hiyo, kufa ni kuishi."
> "Sikuweza kufuata vizuri ufafanuzi wako. Lakini nafikiri katika maneno yako ya mwisho umenivungavunga mahali fulani."
> "Unafikiri unaishi?" aliniuliza.
> "Ndiyo," nilimjibu.
> "Unafikiri kwamba humo katika hali ya kufa?"
> "Hapana"
> "Unafikiri wewe ndiye Kazimoto niliyemwona miaka kadhaa iliyopita? Labda hujitambui. Nakuona umekonda sana siku hizi."
> "Nakubali kwamba nimebadilika."
> "Mabadiliko hayo ndiyo yanakufanya uwe unakufa polepole. Kaburi ni hatua ya mwisho tu ya tendo lilelile."
> "Utaniambia nini juu ya wale wanaokufa wangali bado watoto wadogo?"
> "Wakiwa katika hali hii ya kufa polepole huwa kitu fulani ndani hakiendi sawa. Kwa hiyo, hatua yao ya mwisho inafika kabla ya wakati. Kama uonavyo watu wengine wanapata ndevu wangali na umri wa miaka saba."
>
> (*Kichwamaji,* 1974: 186)

Katika dondoo hili, tunaona Manase ndiye anayetawala zaidi katika mjadala kuhusiana na kifo. Manase anaongea mengi kuhusu kifo. Miongoni mwayo ni kwamba mwanadamu anakufa polepole na kwamba hafi kwa mara moja kama watu wengi wanavyodhani. Manase anaongeza kuwa kaburi ni hatua tu ya kukamilisha tendo lile la kufa polepole kwani tangu mwanadamu alipozaliwa tu na kuendelea kuishi ndivyo siku zake zinavyopungua. Kwa hiyo, mwanadamu yumo katika hali ya kufa na ndiyo maana kwa kadiri siku zake zinavyosonga ndivyo anavyozidi kuwa dhaifu. Kazimoto anakubaliana na mawazo ya Manase kwani yeye mwenyewe anakiri kuwa afya yake siyo kama ilivyokuwa zamani. Hii ni kusema kwamba Kazimoto anakubaliana na wazo kuwa hata yeye yumo katika

hali ya kufa. Aidha, Kazimoto anamuuliza Manase swali kwamba kama mtu anakufa polepole kwa nini watu wengine wanakufa wangali watoto. Manase anamfafanulia kwamba katika hali hiyo ya siku kukatwa polepole kuna mambo yanaweza kutokea ambayo yanamfanya mtoto mdogo afe mapema kama ambavyo mtoto anaweza kuota ndevu akiwa na umri wa miaka saba. Ni katika majadiliano haya, ndipo tunapata kufahamu na kukosolewa kuwa mwanadamu yupo katika hali ya kufa na kwamba kifo hakimpati mwanadamu kama ajali bali humpata taratibu. Hata hivyo, kuna mambo yanayoweza kujitokeza na kumfanya afe kama ajali.

Aidha, mwandishi ametumia mbinu ya mjadala wa wahusika katika ujenzi wa suala la kiuhalisia hakiki katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* (1975) ambalo ni furaha. Kwa mfano, mwandishi anawapambanisha Dennis na Tumaini katika mjadala kuhusu furaha hapa duniani. Ni katika mjadala huu ndipo mwandishi anaonesha unyonge wa mwanadamu katika kuisaka furaha. Katika msako huo mwanadamu ameshindwa kabisa kuipata furaha hapa duniani. Kwa sababu hiyo, ameibua kichwani mwake kitu kinachoitwa mbingu. Rejea mazungumzo ya wahusika hawa katika dondoo lifuatalo katika riwaya ya *Kichwamaji*:

> Mwanadamu ni kiumbe ambaye amejaribu kutafuta njia nyingi zitakazomwezesha kupata furaha. Kwa kuwa ameshindwa kupata furaha hapa duniani amejenga kichwani mwake kitu kama mbingu, yaani mahali anapotegemea kupata furaha baada ya kufa. "Kwa hiyo, wewe unaona kwamba wazo la mbingu limeletwa na kushindwa kwa mwanadamu kupata furaha hapa duniani."
>
> "Ndiyo." (uk. 123)

Katika mjadala wa wahusika hawa ndipo tunabaini fikra za mwandishi kuhusu furaha ambapo anaona kwamba mwanadamu ameshindwa kupata furaha. Pia, katika mjadala huo, mwandishi anafanikiwa kuwakosoa watu wanaoamini kwamba kuna kitu kinachoitwa mbingu ambako ndiko mwanadamu atapata furaha. Mwandishi anawakosoa na kuonesha kwamba mbingu hiyo wameiumba wenyewe kwa sababu ya unyonge wao wa kushindwa kupata furaha hapa duniani.

Aidha, mwandishi anawapambanisha Tumaini na Dennis katika mjadala kuhusu suala la furaha ambapo kupitia mjadala huo tunabaini kwamba mwandishi anakosoa watu wanaodhani kwamba watu wenye furaha ni wale wenye magari, nyumba nzuri na kazi nzuri. Rejea mjadala wao katika dondoo lifuatalo katika *Dunia Uwanja wa Fujo*:

> "Dennis acha uwongo wako; tangu lini ulimwengu ukawa na taabu? Pesa unazo, nyumba na gari unalo, na unaweza kupata karibu kila kitu ukipendacho: taabu uisemayo imetoka wapi? Au labda unamcheka John umaskini. Lakini kama unamwambia John maneno haya mbona yeye anakwenda kufurahi na mwanamke."

> "Tumaini!" Dennis alisema, "Usinione hivi nilivyo ukafikiri kwamba mimi ni mtu mwenye furaha hapa duniani. Nina taabu zangu ambazo labda wewe huwezi kuelewa. (uk. 63)

Dondoo hili linaonesha kuwa Tumaini anaamini mtu mwenye pesa, nyumba na gari basi huyo ana furaha. Dennis anakanusha mawazo hayo kwamba mtu anaweza kuwa na mali yote hiyo lakini bado akawa hana furaha. Ni katika mjadala huu ndipo mwandishi anafanikiwa kukosoa watu wenye fikra kwamba watu wenye mali ndio wenye furaha. Kupitia mjadala huo tunabaini kwamba mwandishi anataka tufahamu kwamba duniani hakuna furaha kwani kila mtu ana shida zake. Utafiti huu unakubaliana na mwandishi kwamba magari, nyumba nzuri na kazi nzuri si ithibati au viashiria tosha vya mtu kuwa na furaha kwani kila mtu ana shida zake.

### 4.1.2 Mbinu ya Matendo ya Wahusika

Utafiti huu umebaini kwamba Kezilahabi katika riwaya zake ametumia matendo ya wahusika katika kujenga masuala yanayojitokeza kiuhalisia hakiki. Mathalani, katika riwaya ya *Kichwamaji* (1974), mwandishi anakosoa mambo mbalimbali kupitia matendo ya wahusika. Kwa mfano, mwandishi anakosoa kitendo cha Rukia kukataa kula mara baada ya kupewa mimba na Manase, jambo lililomsababishia kifo akiwa bado binti. Dondoo lifuatalo linathibitisha hoja hii:

> "Kazimoto," Tuza alisema, "ndugu yako amekufa kwa sababu amekosa nguvu; alikuwa hajala vizuri kwa muda mrefu uliopita."
>
> "Hayo usemayo ni kweli," nilimwambia
>
> "Amekufa akitaja jina lako."
>
> "Alisema nini kuhusu jina langu?"
>
> "Alikulilia; akikuomba umsamehe kwa yale yote yaliyotokea kwake. (uk. 83)

Katika dondoo hili tunaelezwa namna kitendo cha kukataa kula kilivyosababisha kifo cha Rukia. Kupitia kitendo hicho mwandishi anakosoa tabia ya kutokula kwani inaweza kumfanya mhusika kufa kabla ya muda wake. Hii ni kwa sababu mtu hufa polepole, yaani siku zake zinakatwa taratibu lakini akitenda baadhi ya mambo, kifo chake kinaweza kumfikia mapema kuliko ilivyotakiwa. Kwa mfano, kitendo cha Rukia kususa kula ndicho kilichomfanya afe mapema kuliko mama yake, baba yake (Mafuru), wadogo zake kama Kalia na kaka yake (Kazimoto).

Kadhalika, mwandishi anaonesha kuwa matendo ambayo Kazimoto anapaswa kutenda kwenye familia yake yanamsababishia kushindwa kufurahia mapenzi na wasichana. Hili limefanikisha kujenga suala la uhuru wa mwanadamu kiuhalisia hakiki ambapo Kezilahabi anachambua mambo mbalimbali kuhusu uhuru huo na kukosoa masuala ya familia kwa kuonesha kuwa ni moja ya vyanzo

vya mwanadamu kukosa uhuru. Rejea dondoo lifuatalo katika riwaya ya *Kichwamaji* kwa ufafanuzi:

> "Kazimoto, mambo ya wasichana yamekuingilia vile kwamba watu wa nyumbani umewasahau."
>
> “Mambo ya wasichana sihusiani nayo"
>
> "Unasema nini? Mtoto gani wewe? Unataka kunidanganya mimi?
>
> Kazimoto uongo huu wote ulipata wapi? Unafikiri mimi sikukuona unanyatia mihogoni?"
>
> “Basi, basi baba, nisamehe,” nilisema upesi. (uk. 36)

Kupitia matendo ambayo Kazimoto anapaswa kutenda kwa familia yake, mwandishi anachambua na kuona kwamba ndiyo chanzo cha kukosekana kwa uhuru. Hoja hii inatuwezesha kubaini kuwa mwandishi anakosoa jamii na kutaka tuelewe kwamba watu wengi wanatamani kuwa huru lakini wamefungwa na masuala ya kifamilia. Kwa mfano, mtu anaweza kutamani kujenga nyumba nzuri, kumsomesha mtoto wake katika shule nzuri lakini anapotaka kufanya hivyo akikumbuka kwamba ana wazazi wake ambao nao wanatakiwa wafurahi, ana kaka zake, dada zake na wadogo zake ambao wanapaswa kufurahia matunda yake, uhuru wa kufanya baadhi ya mambo hupotea.

Pia, kupitia matendo ambayo mama Kazimoto anataka Kazimoto afanye, mwandishi anakosoa suala la upendo wa wazazi uliopitiliza kwa watoto kwani ndicho chanzo cha kukosekana kwa uhuru. Kwa mfano, mama Kazimoto anamlaumu Kazimoto kwa kitendo cha kuondoka bila kutoa taarifa, naye Kazimoto anamlaumu mama yake kwa kumchunga kama mtoto mdogo. Rejea dondoo lifuatalo katika riwaya *Kichwamaji*:

> Mama aliingia mkono nyuma kama mtu aendaye kilioni. "Ulikuwa wapi?" aliuliza kwa upole.
>
> Mimi nilinyamaza kwa sababu mara nyingi nilikuwa nimemwambia asiniulize swali kama hilo.
>
> "Kazimoto ulikuwa wapi kwa muda wa siku mbili zilizopita? Uliondoka bila kutuarifu na kurudi kwenyewe unarudi usiku wa manane. Umezaliwa, Kazimoto na kuna watu wanaokujali."
>
> "Unataka nini," nilimwambia.
>
> “Kazimoto, fahamu kwamba mimi ninakupenda sana, huwezi kuondoka bila kunipasha habari. Ungeuawa je- tungemshuku nani?”
>
> "Mapenzi ya kitoto namna hiyo, mimi siyapendi. Kila siku niondokapo nyumbani unaniuliza “unakwenda wapi?” Mimi nimekwisha kuwa mtu

> mzima sasa, na sitaki wewe uwe unafahamu njia zangu zote. Hata kama nikiwa nakwenda kwa wanawake unataka nikueleze?" (uk. 64)

Katika dondoo hilo Kazimoto anapigania uhuru wake kutokana na kutokuwa tayari kuuendekeza upendo wa mama yake ambaye anataka kila anachofanya au anapoondoka atoe taarifa. Kupitia matendo ya mama Kazimoto, mwandishi anakosoa tabia ya wazazi kuwapenda watoto wao kupita kiasi, jambo ambalo huwafanya watoto wao waishi kama wafungwa. Hivyo, wazazi wanapaswa kuelewa kwamba si vibaya kumpenda mtoto lakini upendo huo usizidi au kupitiliza, kiasi cha kumchunga mtoto hasa aliyefikia utu uzima.

Zaidi ya hayo, mwandishi ametumia mbinu ya matendo ya wahusika kukemea tabia ya kushiriki mapenzi na makahaba. Kwa mfano, kutokana na kitendo cha Kabenga kushiriki mapenzi na kahaba (Tegemea) alikuwa anamaliza pesa zote alizokuwa anatumiwa na mwanawe (Manase). Rejea dondoo lifuatalo kutoka katika riwaya ya *Kichwamaji* kwa ufafanuzi:

> "Una tamaa sana ya pesa, yaani huwezi kumpenda mtu bila pesa. Huku shamba mwanamke hanunuliwi. Lakini mimi umenimalizia pesa zote anazoniletea mtoto wangu. Hata hivyo, bado hutosheki. Sasa unadai gauni. Unafikiri mimi pesa nazitoa wapi?"
>
> "Kama jambo la gauni limekuudhi vaa suruali yako uende zako! Gauniii! Gauni! Gauni limekuwa gauni. Vaa suruali uende zako! Leo hufanyi jambo lolote nami. Yaani unafikiri mimi maskini omba-omba. Gauni!
> ..." Hasira yote hii ya nini?"
> "Nimesema v-a-a s-u-r-u-a-l-i u-ende zako!"
> Unataka kunitoa nje kana kwamba sikuzaa! Haya chukua!
> "He! He! He!" Tegemea alicheka. "Sasa hizi pesa umezitoa wapi? Bwana'ngu kila siku matata. Ngoja kidogo niweke mto wa pili."
>
> (kur. 70-71)

Dondoo hili linaonesha kwamba Tegemea anamaliza pesa zote za Kabenga bila hata huruma. Kabenga anapojaribu kujitetea kwamba hana hela, anatimuliwa kama mbwa. Kupitia yote haya mwandishi anataka jamii ifahamu kwamba kushiriki mapenzi na kahaba hakufai kwa sababu yeye hana mapenzi ya dhati, anachoangalia ni pesa tu bila kujali huyo anayeshirikiana naye anazipata kwa namna gani. Hivyo, jamii inapaswa kufahamu kuwa kahaba si mke au mume kwamba atamwonea huruma mshirika wake kwamba hana pesa au pesa unazipata kwa namna gani. Suala kama hili tunaliona pia kwa Kalia ambaye anashiriki mapenzi na kahaba huyuhuyu, yaani Tegemea pindi alipojaribu kujitetea kwamba hataweza kupata pesa kwa sababu ya hali ngumu. Tegemea hamwonei huruma licha ya umri wake mdogo, anamwambia kwamba pesa zake zikiisha hatakuwa anashiriki naye mapenzi tena.

Pia, mwandishi ametumia mbinu ya matendo ya wahusika kujenga masuala mbalimbali yanayojitokeza kiuhalisia hakiki katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* (1975). Kwa mfano, kupitia matendo ya Tumaini ya kujisogeza kwa makahaba, mwandishi anakosoa tabia ya wanaume kucheza na makahaba kwani lengo lao huwa ni kuwalaghai wanaume ili wawachune pesa. Rejea dondoo lifuatalo:

> Tumaini alisoma kibao chake *Africans' Royal Bar*. "Karibu humu ndani tupumzike kidogo, Tumaini alimwambia yule msichana. Yule msichana alitazama saa yake. Aliingia hali akijipulizia upepo kwa kitambaa. Alikuwa akitabasamu. Aliwapitisha barabara hiyo makusudi.
> "Unakunywa nini?" Tumaini aliuliza walipokuwa wameingia ndani na kukaa.
> "*Snow cap*" alisema yule msichana.
> "Na John?"
> "Mimi ni ndovu tu."
> Tumaini alitoa noti ya shilingi mia tano, fimbo ya wanaume. Wanawake wa baa waliokuwa wakifanya humo kazi walimtazama mara mbilimbili kwa tabasamu.
>
> (uk. 62)

Dondoo hili linaonesha tamaa ya Tumaini kucheza na makahaba ambapo kahaba alimpitisha baa ili aweze kumnyonya. Isitoshe, baada ya Tumaini kutoa noti ya shilingi mia tano, namna wanawake wa baa walivyoanza kummezea mate ni dhahiri kwamba makahaba lengo lao tu ni pesa. Kwa sababu hiyo, wanaitisha kikao ili kupanga mikakati ya kumnyonya Tumaini pesa zote. Kupitia matendo ya Tumaini na makahaba hawa, mwandishi anakosoa tabia ya wanaume kujihusisha na makahaba kwani tunaona kupitia kitendo cha Tumaini kujihusisha nao, walimmalizia pesa. Dondoo lifuatalo kutoka katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* linathibitisha maelezo haya:

> Walipokuwa wamefika mbali kidogo, Tumaini alianza kusema shida yake. "Siku hizi niko katika hali mbaya sana. Nimejaribu kutafuta kazi lakini sikufanikiwa. Nimekuja kuomba msaada wako, maana ninyi mlioko juu mna nguvu zaidi."
>
> (uk. 81)

Dondoo hili linatuonesha Tumaini akikiri kwamba ana hali mbaya, hali inayorejelewa hapa si ya kiafya bali ni hali ya kiuchumi ambayo ilitokana na kitendo chake cha kutembea na makahaba ambao walimmalizia pesa zake zote licha ya kwamba alikuwa ameachiwa kitita cha pesa na wazazi wake kabla hawajafa. Kupitia matendo ya Tumaini na makahaba hawa ni dhahiri kwamba mwandishi anakosoa tabia ya wanaume kujihusisha na makahaba.

**4.1.3 Mbinu ya Uzungumzinafsiya**

Uzungumzinafsiya ni mtindo wa kuwasilisha mawazo ya mhusika kwa mtindo au njia ya kujizungumzia (Wamitila, 2008). Wamitila anaendelea kueleza kuwa kuna aina mbili za uzungumzinafsiya ambazo ni uzungumzinafsiya wa moja kwa moja, na uzungumzinafsiya usio wa moja kwa moja. Kutokana na kujizungumzia huko kwa mhusika, wasomaji hupata fursa ya kufahamu kile kinachoendelea katika akili ya mhusika. Hivyo, msomaji huweza kubaini sifa au tabia za mhusika huyo pamoja na maudhui yanayoibuliwa. Utafiti huu umebaini kuwa katika riwaya ya *Kichwamaji* (1974), mwandishi ametumia mbinu hii kujenga masuala anuwai yanayojitokeza kiuhalisia hakiki. Miongoni mwa masuala hayo ni kifo ambapo kupitia uzungumzinafsiya wa Kazimoto, mwandishi anatufichulia sababu za Kazimoto kukatisha maisha yake kama inavyojidhihirisha katika ujumbe aliouacha kabla ya kujiua kama unavyoeleza hapa chini:

> Nimejiua. Siwezi kuendelea kuzaa kizazi kibaya. Pia, sikuona tofauti kati yangu na mdudu au mnyama. Akili! Akili! Akili ni nini? Pia, nikiwa duniani sikupata kukutana hata siku moja na mtu anayeamini kwamba kuna Mungu. Watu wanaoogopa kufa na kwenda motoni hao nimewaona, tena wengi sana. Mtu yeyote asilaumiwe kwa kifo changu. Mimi, kabla ya kufa, ninaungama mbele ya ulimwengu kwamba nilimwua mdogo wangu ingawa sikumgusa. (uk. 195)

Katika dondoo hili tunafichuliwa kwamba Kazimoto aliamua kujiua mwenyewe kwa kuogopa aibu ya kuzaa watoto wenye vichwa vikubwa, yaani kizazi kibaya. Kupitia uzungumzinafsiya wa Kazimoto, mwandishi anakosoa jamii na kuitaka ifahamu kwamba matendo maovu yanaweza kumfanya mtu kufa akiwa na umri mdogo. Kazimoto alipata ugonjwa kwa kutembea na Pili ambaye alikuwa kahaba. Matokeo ya ugonjwa huo ni kuzaa watoto wenye vichwa vikubwa ambao yeye anaita kizazi kibaya. Kwa hiyo, kupitia uzungumzinafsiya tunafahamishwa kwamba Kazimoto anajutia juu ya matendo yake ya kushirikiana kimapenzi na kahaba.

Pia, katika uzungumzinafsiya huo mwandishi anakosoa jamii kwa kutufichulia mawazo ya Kazimoto kuwa anajutia matendo yake ya kuendekeza ngono ambayo mdogo wake, Kalia, aliiga na hatimaye kuanza tabia ya ubakaji. Kutokana na tabia hii ya Kalia, baadaye wananchi walishindwa kuivumilia na wakaamua kumuua ili asiendelee kuleta madhara kwa jamii.

Vilevile, mwandishi kupitia mbinu ya uzungumzinafsiya, anatufichulia mawazo ya Kazimoto kuhusu maisha ambapo anakosoa watu wale wanaoona kwamba maisha ni matamu. Kwa upande wake, anaona kwamba maisha ni kama adhabu ambayo Mungu amempa mwanadamu. Kazimoto katika *Kichwamaji* anajisemea:

> Maisha ambayo hayashibwi wala kuridhishwa. Zaidi ya hayo, mwenye nguvu anatunyang'anya maisha haya wakati wowote bila hata

> kutuarifu. Kweli, mfano wa adhabu hii kali ni yule mtu aliyeamrishwa kujaza maji ndani ya pakacha. Na sisi wanadamu tumekubali kufanya hivi kwa jina la 'Furaha'. Maisha matamu! Yaani adhabu ni tamu. Ndiyo kusema tuna akili kweli wanadamu? Maswali haya yalinizunguka sana kichwani. Mara fulani niliamua kwamba mwanadamu hana akili. Kama angekuwa na akili angekataa adhabu hii." (uk. 84)

Katika nukuu hii tunamwona Kazimoto akijizungumzia mwenyewe kuhusu maisha. Kazimoto anajiuliza inakuwaje mwanadamu anayaona maisha matamu. Lengo la mwandishi kutueleza yaliyokuwa kichwani kwa Kazimoto ni kutaka kutufikishia ujumbe kwamba maisha ni kama adhabu tu ambayo mwanadamu amepewa na Mungu. Kwa sababu hiyo, anatilia shaka kama kweli mwanadamu ana akili kama ambavyo yeye mwenyewe anajiona. Hii ni kwa sababu amekubali adhabu ya kuyatunza maisha. Isitoshe, anayafurahia kwa kusema kuwa maisha ni matamu. Mwandishi anaona kwamba kama mwanadamu angekuwa na akili kweli lazima angeikataa adhabu hiyo. Kitendo cha kuikubali adhabu hiyo kinampa shaka mwandishi ikiwa kweli mwanadamu ana akili.

Pia, kupitia uzungumzinafsiya wa Kazimoto, mwandishi anasaili maisha ya mwanadamu hapa duniani kwa kutufichulia kuwa maisha hayana faida yoyote kwa sababu mwanadamu anachofaidi kwa kuishi ulimwenguni ni kukusanya taka mbalimbali zilizopo duniani. Taka hizi ni kama magonjwa, chuki, visasi, msongo wa mawazo, aibu na fedheha. Kazimoto katika *Kichwamaji* anaeleza:

> Niliona kwamba mwanadamu anateremka kama maji kwa kasi sana; na kama maji ya mto yakusanyavyo takataka za kila aina ndivyo mwanadamu akusanyavyo taka wakati wa maisha yake. Maji yakifika ziwani yamekwisha kusanya taka nyingi; pia mwanadamu afikapo mwishoni mwa maisha yake huwa amekusanya taka kadiri ya muda alioishi. Niliona heri ningekufa ningali mtoto. (uk. 90)

Katika dondoo hili, tunamuona Kazimoto akizungumza mwenyewe nafsini mwake na kuona kwamba hakuna faida yoyote ya kuishi. Mawazo haya ni tofauti na ya watu wengine ambao wanatamani Mungu awape maisha marefu. Kwa upande wa Kazimoto, hali ilikuwa tofauti, yeye anaona ni bora angekufa angali mtoto kabla ya kukusanya takataka nyingi za hapa duniani. Kupitia uzungumzinafsiya huu mwandishi amefanikisha kuwasilisha suala la maisha kiuhalisia hakiki kwa kuchambua, kusaili na kukosoa mawazo mbalimbali yaliyopo miongoni mwa wanajamii walio wengi kuhusu maisha ya mwanadamu. Mbatiah (1998) anadokeza suala hili ambapo anasema kwamba Kezilahabi ametumia sana uzungumzinafsiya kupitia mhusika Kazimoto katika kufichua masuala mbalimbali kama vile maana ya maisha. Hata hivyo, Mbatiah anadokeza tu kwamba mtindo huu umetumiwa na mwandishi wa riwaya hii ya *Kichwamaji* (1974) bila kuonesha umetumika wapi na alikuwa anazungumzaje huyo Kazimoto. Utafiti huu umeenda

mbele zaidi kwa kuuchambua mtindo huu na kuuonesha ulitumiwa sehemu gani na ulikuwa unazungumzia kitu gani.

### 4.1.4 Mbinu ya Sitiari

Sitiari ni kipengele kinachohusisha uhamishaji wa maana kutoka kikoa kimoja kwenda kingine (Leech, 1969 na 1981). Kwa mantiki hii, sitiari huunganisha vikoa viwili vya maana. Hata hivyo, ikumbukwe kuwa muunganisho huu si kamili kwa sababu wakati huohuo kuna ukanusho wa muunganisho huo, yaani usitiari wa kiambo kitokanacho na muunganisho huo hutegemea upambanufu baina ya vipengele vyake. Kwa mfano, tunaposema "K ni simba" tunaunganisha vikoa viwili vya "binadamu na mnyama", kwa maana kwamba (maana au sehemu ya maana) maana ya "simba" imehamishiwa kwenye "binadamu". Hata hivyo, bado K si simba, na huo ndiyo ukanusho wenyewe unaozungumziwa. Utafiti huu umebaini kwamba Kezilahabi ametumia mbinu hii katika kujenga masuala yanayojitokeza kiuhalisia hakiki. Kwa mfano, katika riwaya ya *Kichwamaji* (1974), mwandishi ametumia sitiari ambapo anafananisha maji yateremkayo kuelekea ziwani yanavyokusanya taka na maisha ya mwanadamu yalivyo. Mwandishi ametumia sitiari hiyo kuchambua na kukosoa mawazo ya wengi kwa kusema kwamba maisha ya mwandamu hayana maana yoyote, na kwamba mtu anayeishi miaka mingi hana anachomzidi yule aliyekufa mapema zaidi ya kukusanya taka kama vile chuki, magonjwa, msongo wa mawazo na visasi. Kwa sababu hiyo, mwandishi anaona kwamba ni heri angekufa angali mtoto. Dondoo lifuatalo linathibitisha maelezo haya:

> Niliona kwamba mwanadamu anateremka kama maji kwa kasi sana; na kama maji ya mto yakusanyavyo takataka za kila aina ndivyo mwanadamu akusanyavyo taka wakati wa maisha yake. Maji yakifika ziwani yamekwisha kusanya taka nyingi; pia mwanadamu afikapo mwishoni mwa maisha yake huwa amekusanya taka kadiri ya muda alioishi. Niliona heri ningekufa ningali mtoto. (uk. 90)

Sitiari iliyotumika katika dondoo hili inatupa picha kwamba msanii haoni maana ya maisha zaidi ya kukusanya taka pindi anaposubiri kifo. Pia, mwandishi ametumia sitiari ya 'miaka ni kama kunguni' katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* (1975), kuchambua na kukosoa wanajamii kuhusu suala la kwamba mwanadamu anakufa kama ajali. Dondoo lifuatalo linaonesha sitiari hiyo:

> Mungere hakunung'unika: alifahamu kwamba mumewe hakuwa mvivu. Alifahamu kwamba miaka ni kama kunguni; inamnyonya mtu pole pole, halafu huacha gofu kuanguka kaburini. (uk. 6)

Kupitia sitiari hii, tunaona mwandishi anafananisha idadi ya miaka ya mwanadamu inavyomfanya awe dhaifu polepole kama ambavyo kunguni humnyonya mnyama polepole bila yeye mwenyewe kufahamu. Sitiari hii inatumika kuonesha kwamba

mwanadamu anakufa polepole na si kama watu wanavyofikiri kwamba mtu hufa mara moja, yaani kama ajali.

#### 4.1.5 Mbinu ya Uwasilishaji Dhahiri

Uwasilishaji dhahiri ni mbinu ya kuwasilisha maudhui bila kutumia mbinu za tamathali za semi kama vile sitiari, tasfida, tashbiha, taswira na tashititi. Mbinu hii humsaidia msomaji au hadhira kutopata taabu ya kubaini maudhui ya kazi husika. Utafiti huu umebaini kwamba Kezilahabi katika riwaya zake teule ametumia mbinu ya uwasilishaji dhahiri ili kujenga masuala anuwai yanayojitokeza kiuhalisia hakiki. Kwa mfano, katika riwaya ya *Kichwamaji* (1974) mwandishi ametumia uwasilishaji dhahiri kukosoa mawazo ya waumini wa Kikristo na Kiislamu wanaomchukulia Mungu kama ni mwenye huruma. Kwa upande wake anamuona Mungu kama katili bila hata kutumia angalau tamathali ya semi ili kupunguza ukali wa kauli kama hiyo. Rejea dondoo lifuatalo kwa ufafanuzi:

> Usiku nikiwa na mke wangu, mawazo mengi yalinijia kichwani. Nilianza tena kufikiri juu ya Mungu. Kama kweli Mungu alikuwapo sikuona kwa nini aliweza kufanya ukatili mkubwa kama huo. Matumaini yetu yote; kazi na taabu tuliyopata-yote hayo chini! Sikuona maana ya maisha. (uk. 180)

Dondoo hili linaeleza waziwazi namna Mungu anavyofanya ukatili kwa kuzimisha matumaini ya mwanadamu bila kujali taabu zake. Katika riwaya hiyo, tunasimuliwa na Kazimoto kwamba matumaini yote ya kupata mtoto, taabu yote ya kulea mimba hadi kufikisha miezi tisa ilizimishwa na Mungu kwa kumuua mtoto wao ambaye aliishi kwa saa moja tu baada ya kuzaliwa. Pia, katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* (1975), mwandishi ametumia mbinu ya uwasilishaji dhahiri kukosoa watu wanaodhani kwamba mtu akiwa na pesa, nyumba na gari, basi huyo ndiye mwenye furaha. Rejea dondoo lifuatalo:

> “Dennis acha uwongo wako; tangu lini ulimwengu ukawa na taabu? Pesa unazo, nyumba na gari unalo, na unaweza kupata karibu kila kitu ukipendacho: taabu uisemayo imetoka wapi? Au labda unamcheka John umaskini. Lakini kama unamwambia John maneno haya mbona yeye anakwenda kufurahi na mwanamke.”
>
> “Tumaini!” Dennis alisema, “Usinione hivi nilivyo ukafikiri kwamba mimi ni mtu mwenye furaha hapa duniani. Nina taabu zangu ambazo labda wewe huwezi kuelewa. (uk. 63)

Katika dondoo hili mwandishi anakosoa waziwazi fikra za watu wengi wanaodhani kwamba mtu mwenye pesa, nyumba na gari ndiye mwenye furaha. Mwandishi kwa upande wake, anaona kuwa hata huyo naye ana taabu zake. Kwa mantiki hiyo, tunaweza kusema kuwa mwandishi anaona hakuna mtu mwenye furaha hapa duniani. Katika sehemu hii ya makala tumeona mbinu mbalimbali zilizotumika kujenga masuala yanayojitokeza kiuhalisia hakiki katika riwaya teule

za Euphrase Kezilahabi. Uchambuzi wa mbinu hizo umedhihirisha madai ya msingi mkuu wa mkabala wa nadharia ambao ni kuchambua, kusaili na kukosoa hali iliyopo katika jamii. Kupitia mbinu hizo tumeona namna mwandishi alivyochambua, kusaili na kukosoa mambo mbalimbali katika jamii. Katika sehemu inayofuata tumechambua dhima za mtindo wa uhalisia hakiki katika riwaya za *Kichwamaji* (1974) na *Dunia Uwanja wa Fujo* (1975) za Euphrase Kezilahabi.

## 4.2 Dhima za Mtindo wa Uhalisia Hakiki katika Riwaya Teule za Euphrase Kezilahabi

Katika kuchambua dhima za mtindo wa uhalisia hakiki kwenye uandishi wa riwaya tumeongozwa na Mkabala wa Uhalisia Hakiki ambao unasema kwamba waandishi wa mtindo wa uhalisia hakiki hawaishii tu kusawiri hali kama ilivyo katika jamii, bali wanachambua, wanakosoa na kusaili hali hiyo. Hivyo, kwa kuzingatia kipengele cha uchambuzi kwenye mkabala husika tumebaini kwamba mtindo huu una dhima mbalimbali kama zinavyofafanuliwa kwenye sehemu ndogondogo zifuatazo.

### 4.2.1 Kumpambanua Msanii

Kipengele ambacho kinampambanua msanii baina ya wasanii wengine ni mtindo. Senkoro (1982) anaeleza kuwa mtindo ni upangaji wa fani na maudhui katika kazi ya fasihi kwa njia ambayo hutokeza au huonesha nafasi na labda upekee wa mtunzi wa kazi hiyo. Naye Wamitila (2003) anaeleza kuwa mtindo hurejelea sifa maalumu za mwandishi au mazoea ya mwandishi fulani ambaye hujionesha kwenye fani yake. Mazoea hayo ya kuandika, kuteua msamiati, tamathali za semi, taswira, uakifishaji, sentensi, na kadhalika, ndiyo yanayompambanua mwandishi mmoja na mwingine. Wataalamu hawa wanadhihirisha kwamba mtindo ndicho kipengele ambacho hufanya kazi ya kumtofautisha msanii wa kazi moja na nyingine. Pia, katika utafiti huu tumebaini kwamba mtindo wa uhalisia hakiki, umeonesha dhima ya kumtofautisha Kezilahabi na waandishi wengine wa riwaya ya Kiswahili. Mathalani, katika uchambuzi wa maana ya maisha, mtindo huu umetumiwa na mwandishi ili kumpambanua miongoni mwa waandishi wengine ambao wameishia tu kusawiri maisha kama yalivyo, bila kuchambua maana yake. Kwa mfano, katika riwaya ya *Kichwamaji* (1975), mwandishi anayaona maisha ya mwanadamu hayana maana yoyote. Kupitia mhusika Kazimoto, Kezilahabi anasema:

> Usiku nikiwa na mke wangu, mawazo mengi yalinijia kichwani. Nilianza tena kufikiri juu ya Mungu. Kama kweli Mungu alikuwapo sikuona kwa nini aliweza kufanya ukatili mkubwa kama huo. Matumaini yetu yote; kazi na taabu tuliyopata-yote hayo chini! Sikuona maana ya maisha. (uk. 180)

Katika dondoo hilo baada ya Kazimoto kupitia masaibu mbalimbali ikiwamo kufiwa na mtoto wake ambaye aliishi saa moja tu baada ya kuzaliwa, anasema hakuona maana ya maisha. Mtazamo huu wa kuyaona maisha hayana maana umempambanua Kezilahabi kwa kiwango kikubwa katika fasihi ya Kiswahili. Pia, mwandishi ameyachambua maisha ya mwanadamu na kubaini kuwa ni kama fujo za muda fulani. Mtazamo huu wa kuyaona maisha ya mwanadamu kama fujo tu zenye ukomo umempambanua msanii huyu miongoni mwa waandishi wengine wa fasihi ya Kiswahili kama vile Shaaban Robert na Shafi Adamu Shafi ambao wameishia tu kusawiri suala hili bila kuchambua maana yake. Dondoo lifuatalo kutoka katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* linathibitisha hoja hii:

> Zamani, niliamini kwamba kila mwanadamu ameumbwa kuja hapa duniani ili apate kufurahia ulimwengu kiasi awezavyo kabla hajafa. Lakini sasa ninaamini kwamba **Dunia Uwanja wa Fujo**. Kila mwanadamu ameumbwa kuja kufanya fujo yake halafu anajiondokea na kupotea. Kuna fujo za aina nyingi. Watu wengine wamefanya fujo zaidi ya wengine. (uk. 63)

Mwandishi katika dondoo hilo haishii tu kusawiri maisha kama yalivyo, bali ameyachambua na kubaini kuwa ni fujo tu ambazo mwanadamu ameumbwa ili azifanye na muda wake ukiisha apishe na wengine. Uchambuzi wa namna hii wa maisha, umesaidia kumpambanua Kezilahabi miongoni mwa waandishi wengi wa fasihi ya Kiswahili. Kwa kuzingatia kipengele cha uchambuzi kwenye msingi mkuu wa mkabala wa nadharia ambao ni kuchambua, kusaili na kukosoa hali iliyopo katika jamii, tumeweza kubaini dhima ya kumpambanua msanii atumiapo mtindo wa uhalisia hakiki.

### 4.2.2 Kumtafakarisha Msomaji

Utafiti umebaini kwamba mtindo wa uhalisia hakiki una dhima ya kumtafakarisha msomaji wa kazi hizo. Hii ni kwa sababu kwa kutumia mtindo huu, Kezilahabi anachambua masuala mbalimbali ambayo yanamfanya msomaji atafakari kuhusu yale yanayoelezwa na yale ambayo yapo katika jamii. Kwa mfano, wakati katika jamii watu wanaamini kwamba kuna mbingu kutokana na mafundisho ya dini ya Kikristo. Kupitia mtindo huu mwandishi anaeleza kuwa mbingu ni dhana tu ambayo imejengwa na mwanadamu baada ya kushindwa kupata furaha hapa duniani. Kwa hiyo, amejenga dhana hiyo kwa kujipa moyo kwamba huko mbinguni ndiko atapata furaha mara baada ya kufa. Katika riwaya ya *Kichwamaji* mhusika kupitia Manase, Kezilahabi anatueleza:

> Mwanadamu ni kiumbe ambaye amejaribu kutafuta njia nyingi zitakazomwezesha kupata furaha. Kwa kuwa ameshindwa kupata furaha hapa duniani amejenga kichwani mwake kitu kama mbingu, yaani mahali anapotegemea kupata furaha baada ya kufa. “Kwa hiyo,

> wewe unaona kwamba wazo la mbingu limeletwa na kushindwa kwa mwanadamu kupata furaha hapa duniani."
>
> "Ndiyo." (uk 123)

Dondoo hili linaonesha kwamba mbingu ni dhana tu iliyoundwa na mwanadamu kwa kujifariji. Kimsingi, hali kama hii humfanya msomaji atafakari tena kuhusu suala la mbingu na hatima yake baada ya kifo. Vilevile, kupitia mtindo huu wa uhalisia hakiki, mwandishi anamtafakarisha msomaji ambapo tunaona wahusika wawili, Tumaini na Dennis, wakiwa katika mjadala kuhusu furaha katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* (1975). Katika mjadala huo, Tumaini anaamini kwamba mtu mwenye furaha ni yule mwenye pesa, gari na nyumba na yule mwenye uwezo wa kukipata kila akitakacho wakati Dennis anasema kwamba hata mwenye vitu hivyo hana furaha kwani naye ana taabu zake. Rejea mjadala wao katika dondoo lifuatalo:

> "Dennis acha uwongo wako; tangu lini ulimwengu ukawa na taabu? Pesa unazo, nyumba na gari unalo, na unaweza kupata karibu kila kitu ukipendacho: taabu uisemayo imetoka wapi? Au labda unamcheka John umaskini. Lakini kama unamwambia John maneno haya mbona yeye anakwenda kufurahi na mwanamke."
>
> "Tumaini!" Dennis alisema, "Usinione hivi nilivyo ukafikiri kwamba mimi ni mtu mwenye furaha hapa duniani. Nina taabu zangu ambazo labda wewe huwezi kuelewa. (uk. 63)

Mazungumzo baina ya wahusika hawa humfanya msomaji atafakari zaidi kuhusu suala la furaha. Msomaji atafikiri mara mbilimbili kati ya hao nani yupo sahihi na pengine kujitazama yeye mwenyewe ikiwa ana furaha au hana. Ikiwa hana, kwa nini? Je, akiwa na gari, nyumba na pesa atakuwa na furaha? Kama atakuwa nayo furaha hiyo, je, Dennis ni mwongo anayesema licha ya kuwa na gari na pesa, bado hana furaha? Kwa ujumla, mtindo huu hutumiwa na mwandishi ili msomaji atafakari masuala mbalimbali yanayomzunguka na hatima yake baada ya kifo.

### 4.2.3 Kujenga Jamii Mpya

Utafiti huu umebaini kwamba ujenzi wa jamii mpya ni miongoni mwa dhima za mtindo wa uhalisia hakiki katika riwaya teule. Hii ni kwa sababu katika mtindo huu mwandishi hukosoa baadhi ya mambo yanayoendelea katika jamii. Kwa mfano, mwandishi anakosoa tabia za wanaume kushirikiana kimapenzi na makahaba kwa sababu kuna madhara makubwa ya kufanya hivyo. Mathalani, kupitia uhusianao wake wa kimapenzi na Tegemea ambaye ni kahaba, Kabenga anamaliza pesa zote anazotumiwa na mwanawe (Manase). Vilevile, Kabenga hata pale anapojaribu kujitetea kuwa pesa zote amemmalizia, Tegemea anamfukuza kama mbwa. Dondoo lifuatalo linathibitisha hoja hii:

> "Una tamaa sana ya pesa, yaani huwezi kumpenda mtu bila pesa. Huku shamba mwanamke hanunuliwi. Lakini mimi umenimalizia pesa zote anazoniletea mtoto wangu. Hata hivyo, bado hutosheki. Sasa unadai gauni. Unafikiri mimi pesa nazitoa wapi?"
> "Kama jambo la gauni limekuudhi vaa suruali yako uende zako! Gauniii! Gauni! Gauni limekuwa gauni. Vaa suruali uende zako! Leo hufanyi jambo lolote nami. Yaani unafikiri mimi maskini omba-omba. Gauni!
> … "Hasira yote hii ya nini?"
> "Nimesema v-a-a s-u-r-u-a-l-i u-ende zako!"
> Unataka kunitoa nje kana kwamba sikuzaa! Haya chukua!
> "He! He! He!" Tegemea alicheka. "Sasa hizi pesa umezitoa wapi? Bwana'ngu kila siku matata. Ngoja kidogo niweke mto wa pili." (kur. 70-71)

Dondoo hili linaonesha kwamba mwandishi anakosoa tabia za wanaume kushirikiana kimapenzi na makahaba. Lengo la ukosoaji huu ni kujaribu kujenga jamii mpya ambayo mwanamume akitaka mapenzi atayapata kutoka kwa mkewe na si kwa kahaba kama anavyofanya Kabenga na wahusika wengine kama Kazimoto na Manase.

Pia, katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* (1975), mwandishi anakosoa tabia ya Tumaini kushirikiana kimapenzi na makahaba wa *Africans' Royal Bar* kwa kuonesha madhara yake. Kwanza, makahaba hao walimwandalia mkutano wa kumnyonya pesa yote. Rejea dondoo lifauatalo linaloeleza mpango huo wa makahaba:

> "Hivi kati yetu Tumaini anamtaka nani?" Fatuma aliuliza.
>
> "Hadija!" wote walipiga kelele.
>
> "Basi tumwache," Fatuma alisema, "tumwache aendeshe mambo. Tukipinduliana serikali hatuwezi kufika mbali.
>
> Ni Tumaini ambaye anaweza kutoa pesa kwa wingi. Yule msichana mjinga wa kwao [mke wa Tumaini, Anastansia] hafai kula pesa hizo peke yake." Huo ndio ulikuwa mkutano uliohusu jinsi ya kumnyonya vizuri Tumaini. (uk. 74)

Dondoo hilo linaonesha mpango wa makahaba wa kuhakikisha wananyonya pesa zote za Tumaini, bila kujali kwamba ana mke wake ambaye anamtegemea pamoja na familia yake. Makahaba hao walifanikisha mpango wao kwani katika ukurasa wa 81, Tumaini anamweleza Dennis kwamba sasa yupo katika hali mbaya; kwa hiyo, anamuomba Dennis amtafutie kazi. Yote haya mwandishi anayaeleza kupitia mtindo wa uhalisia hakiki ili kujenga jamii mpya, kwa maana kwamba msomaji asithubutu kushirikiana kimapenzi na makahaba, na hatimaye kujenga familia zilizo imara. Kupitia ujenzi wa jamii mpya kama dhima mojawapo ya matumizi ya

mtindo wa uhalisia hakiki kwenye uandishi, tumeweza kuibaini kwa kuzingatia kipengele cha uchambuzi kwenye msingi mkuu wa mkabala husika.

#### 4.2.4 Kuibua Mambo Mapya

Utafiti huu umebaini kwamba miongoni mwa dhima za mtindo wa uhalisia hakiki ni kuibua mambo mapya. Kupitia uchambuzi, ukosoaji na usaili wa mambo yanayoendelea katika jamii, mwandishi hujikuta anaibua mambo mapya ambayo hayapo katika jamii au hata kama yapo katika jamii, basi wanajamii walikuwa hawajui jinsi gani yalivyo. Kwa mfano, katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* (1975), mwandishi kupitia mtindo wa uhalisia hakiki anaibua jambo jipya ambalo hata katika jamii si rahisi kulikuta. Jambo hilo ni wazo kwamba wema (waliotenda mema hapa duniani) hawaendi mbinguni. Kwa mujibu wa mwandishi, maisha ya mwanadamu ni kama jani, likishadondoka kutoka mtini basi halitarudi tena, na ndivyo maisha ya mwanadamu yalivyo: akifa amekufa, awe mwema au mwovu, hawezi kuwa na maisha tena. Dondoo lifuatalo linathibitisha hoja hii:

> "Zamani," Dennis alisema, hata mimi nilifikiri kwamba maisha mazuri sana, na kwamba watu wema huenda mbinguni; lakini sasa nina mawazo tofauti kabisa na yale ya zamani. Ulimwengu siku hizi ninauona kama meza-kama meza hii ya kulia unayoiona sasa. Sisi wanadamu tu kama majani. Tunaanguka kutoka juu mtini; tunakuja tunapepea angani kama unyoya namna hii na kuanguka juu ya meza ta! Hakuna atakayerudi juu mtini. (uk.64)

Katika dondoo hili, mwandishi anaibua jambo jipya kwa kusema kwamba zamani alifikiri watu wema huenda mbinguni lakini sasa ana mawazo tofauti. Hii ina maana sasa hivi haamini kama watu wema huenda mbinguni. Wazo kama hili ni jipya kwa sababu kulingana na mafundisho ya dini ya Kikristo watu wema wataenda mbinguni huku waovu wakitupwa katika tanuri la moto (jehanamu). Hii ina maana kwamba kupitia mtindo huu wa uhalisia hakiki mwandishi huepuka ukasuku katika uandishi wake ambapo huwa anaibua mambo yaliyo mapya. Kwa mujibu wa Kezilahabi (2003), ukasuku ni hali ya kuandika kitu bila kufikiri sana, yaani hali ya kurudia mawazo yaliyokwishaandikwa na wengine au kurudia maneno yanayosemwa na wanasiasa bila fikra mpya na pengine hata kuyarudia isivyo kwa njia ya kuupotosha umma. Kezilahabi anaongeza akisema kuwa hatari kubwa ya ukasuku ni kwamba unadhalilisha uwezo wa mwandishi kuona mbele. Yumkini ni kwa sababu hiyo Kezilahabi katika riwaya zake anaibua mambo mapya ambayo hayakupata kuandikwa ili kuepuka kujidhalilisha kwa kurudia yale yaliyokwishazungumzwa na waandishi wengine. Kwa kuzingatia kipengele cha uchambuzi kwenye msingi mkuu wa mkabala wa nadharia ambao ni kuchambua, kusaili na kukosoa hali iliyopo katika jamii, tumeweza kubaini dhima ya kuibua mambo mapya katika jamii.

**5.0 Hitimisho**

Makala hii ni matokeo ya utafiti uliofanyika kuchunguza mbinu za ujenzi wa masuala ya kiuhalisia hakiki na dhima zake katika riwaya za *Kichwamaji* (1974) na *Dunia Uwanja wa Fujo* (1975) za Euphrase Kezilahabi. Matokeo yameonesha kwamba, mbinu tano zimetumika kujenga masuala hayo. Mbinu hizo ni majadiliano baina ya wahusika, matendo ya wahusika, uzungumzinafsiya, sitiari na uwasilishaji dhahiri. Kwa upande mwingine, dhima za mtindo huo ni kumpambanua msanii, kumtafakarisha msomaji, kujenga jamii mpya na kuibua mambo mapya.

## Marejeleo

Arabi, S., Moghbel, A.G., Zareh, N., Balawi, R. na Pourabed, M.J. (2022). "A Comparative Study of the Aspects of Critical Realism between *Yiki Boud Yaki Nabud* of Muhammad Ali Jamalzadeh and *Kan Ma Kan* by Mikhail Naima." *Biannual Journal*. 25(2): 135-167. Inapatikana katika https://doi.org/10.30465 /afg.2022.6771. Ilisomwa tarehe 10 Januari 2023.

Bhasker, R. (2007). *Enlightened Common Sense: The Philosophy of Critical Realism*. London: Routledge.

Gorky, M. (1949). *Mother*. Moscow: Progress Publishers.

Kezilahabi, E. (1971). *Rosa Mistika*. Dar es Salaam: East African Literature Bereau.

Kezilahabi, E. (1974). *Kichwamaji*. Dar es Salaam: East African Publishing House

Kezilahabi, E. (1975). *Dunia Uwanja wa Fujo*. Nairobi: Vide~Muwa Publishers.

Kezilahabi, E. (1979). *Gamba la Nyoka*. Dar es Salaam: East African Publishers.

Kezilahabi, E. (1990). *Nagona*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Kezilahabi, E. (1991). *Mzingile*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Kezilahabi, E. (2003). "Utunzi wa Riwaya na Hadithi Fupi." Katika *Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili III*. Dar es Salaam. TUKI. Kur. 226-243.

Laird, A. (2006). *Ancient Literary Criticism*. Oxford: Oxford University Press.

Leech, G.N. (1969). *A Linguistic Guide to English Poetry*. Newyork: Longman.

Leech, G.N. (1981). *Semantics: The Study of Meaning*. London: Penguin Books.

Madumulla, J.S. (2009). *Riwaya ya Kiswahili; Nadharia, Historia na Misingi ya Uchambuzi*. Dar es Salaam: Mture Educational Publishers Limited na Nairobi: Phoenix Publishers Limited.

Mbatiah, M. (1998). "Mienendo Mipya katika Uandishi wa Kezilahabi: *Nagona* na *Mzingile*." *Mulika*, 24: 1-13.

Mlacha, S.A.K na Madumulla, J.S. (1991). *Riwaya ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Mulokozi, M.M. (2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: KAUTTU.

Quayson, A. (2000). *Postcolonialism: Theory, Practice or Process*. Cambridge: Polity Press.
Senkoro, F.E.M.K. (1982). *Fasihi*. Dar es Salaam: Press and Publicity Centre.
Senkoro, F.E.M.K. (1995). "Euphrase Kezilahabi: Shaaban Robert wa Pili." *Kioo cha Lugha*.1: 61-69.
Vasquez, A.S. (1973). *Art and Society*. Newyork: Monthly Review Press.
Wamitila, K.W. (2003). *Kamusi ya Fasihi. Istilahi na Nadharia.* Nairobi: Focus Publications Limited.
Wamitila, K.W. (2008). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide~Muwa Publishers.